Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

Laylatul-Qadr na I'tikaaf

17th Ramadhaan 1431
27th August, 2010

Volume 1, Issue 4

Yaliyomo

Laylatul-Qadr 1-2
I'tikaaf 2-3
Ukumbi wa Kina mama 4

Laylatul-Qadr (Usiku ulio barikiwa)

Fadhla zake ni kubwa, kwani katika usiku huu Qur'an Tukufu iliteremshwa, ambayo ndiyo yenye kumuongoza mwenye kushikamana nayo kwenye njia ya Utukufu na heshima, na Qur'an hiyo itamuinua kwenye kilele cha Utukufu na kuwa na maisha ya Milele. Waislamu wenye kufuata Sunnah za Mtume ((صلى الله عليه وسلم) kikamilifu, hawainui bendera katika usiku huu, wala hawaangiki mapambo ya kumeremeta. Bali wanashindana katika kusimama ufikapo wakati huo (wa Laylatul-Qadr) kwa ajili ya kuswali kutokamana na imani na wakiwa na matarajio ya malipo mema. Hapa, Ewe Muislamu, kuna aya za Qur'an na hadeeth zilizo swaheeh za Mtume (صلى الله عليه وسلم) zenye kuhusiana na usiku huu.

• Fadhla za Laylatul-Qadr

Ama kuhusu fadhla zake, inatosha kutaja yakwamba Laylatul-Qadr ni bora kuliko miezi elfu moja. Amesema (عز وجل):

"Hapana shaka tumeiteremsha Qur'an katika usiku wa cheo. Na ni jambo gani linalokujuza ni nini usiku wa cheo? Usiku wa cheo ni bora kuliko miezo elfu moja. Huteremka Malaika na Jibreel katika usiku huo kwa ruhusa ya Mola wao kwa kila jambo. Amani, usiku huo mpaka kuingia alfajiri. [al-Qadr 97: 1-5]

Na katika usiku huo, Allaah hubainisha kila jambo. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى):

"Hapana shaka sisi tumeiteremsha Qur'an katika usiku wenye kubarikiwa. Hapana shaka sisi ni wenye kuwakhofisha waja katika usiku wenye cheo huwekwa wazi kila jambo lilohukumiwa (kama riziki, ajali, n.k). mambo yanayotoka kwetu. Hapana shaka sisi tulikuwa ni wenye kupeleka Mitume. Kwa ajili ya huruma inayotoka kwa Mola wako. Hapana shaka Yeye (Allaah) ni Mwenye kusikiya, Mjuzi. [ad-Dukhaan 44:3-6]

• Ni Wakati Gani?

Imepokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba usiku huu umo ndani ya tarehe ishirini na moja, ya ishirini na tatu, ya ishirini na tano, ya ishirini na saba, ya ishirini na tisa au ndani ya usiku wa mwisho wa Ramadhaan. Amesema Imaam ash-Shaafi'ee (رحمه الله): *"Kana kwamba jambo hili kwangu mimi, na Allaah yamueleya yakwamba* Mtume (صلى الله عليه وسلم) *alikuwa akijibu masuali kulingana na suali liulizwavyo."* Alikuwa akiulizwa, *"Jee, niutafute katika usiku kadhaa na kadhaa?"*, nae hujibu, *"Utafute kwenye usiku fulani na fulani."*

Na kauli yenye nguvu ni kwamba hutokeya katika siku za witr za kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhaan na dalili ya haya ni hadeeth ya 'Aaisha (رضي الله عنها) amesema: *"Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya i'tiqaaf kwenye siku kumi za mwisho, na akisema: "Itafuteni Laylatul-Qadr katika (siku za witr) za kumi la mwisho wa Ramadhaan."*

Hata hivyo, iwapo mja atadhoofika au atashindwa, basi angalau asiziwache siku saba za mwisho kumpita, kutokana na yaliyopokewa kutoka kwa Ibn 'Umar, aliyesema: *"Amesema Mtume* (صلى الله عليه وسلم): *"Itafuteni katika siku kumi za mwisho, na iwapo mmoja wenu atadhoofika au atashindwa, basi angalau asiziwache siku saba zilizobaki kumpita.'"*

Hadeeth hii inafafanua matamshi yake (صلى الله عليه وسلم): *"Naona ndoto zenu zimeafikiana (yakwamba inapatikana katika siku saba za mwisho) kwahivyo yule anaetaka kuutafuta usiku wa L:aylatul-Qadr, autafute kwa kujitahidi na Ibada katika siku saba za mwisho."*

Na ni jambo lenye kujulikana katika Sunnah, yakwamba hakika ya ujuzi wa usiku huo ambayo Laylatul-Qadr hushuka ulipaazwa kwa sababu watu walikuwa wakigombana na kuteta. Amesema 'Ubaadah ibn as-Saamit (رضي الله عنه): *"Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *alitujilia kutaka kutuelezea kuhusu Laylatul-Qadr, kukawa na watu wawili wakiteta nae akasema: 'Mimi nimekuja kutaka kuwaelezea kuhusu Laylatul-Qadr, lakini fulani na fulani, na fulani na fulani walikuwa wakiteta, mara ikarufaishwa juu, na pengine hiyo ilikuwa ni kheri kwenu, basi itafuteni katika usiku wa (ishirini na) tisa, na (ishirini na) saba, na (ishirini na) tano.'"*

Baadhi ya ahaadeeth zinaashiriya yakwamba Laylatul-Qadr inapatikana katika usiku wa siku kumi za mwisho, na nyengine zinaashiriya yakwamba inapatikana katika usiku wa siku kumi za witr, kwahivyo, katika riwaya ya kwanza ilikuwa ni kwa ujumla na hiyo riwaya nyengine ilikuwa ni makhsusi, na makhsusi hutangulizwa kuliko ya ujumla. Ahaadeeth nyengine zaonyesha yakwamba usiku huu wapatikana katika siku saba za mwisho – na hukmu hizi zimefungwa kwa kutaja aliyedhaifu au asiyejiweza. Kwahivyo hakuna mushkil wowote, ahaadeeth zote zinaafikiyana na wala hazikukhitilafiana.

Kwa kumalizia: Muislamu na ajitahidi katika kuitafuta Laylatul-Qadr katika siku za witr za kumi la mwisho: usiku wa ishirini na moja, na

1. Kutakuwa na Darsa za wanawake katika mwezi wa Ramadhaan, msikiti wa Mazrui, kuanzia saa Nne asubuhi mpaka Adhuhuri—kila siku isipokuwa Ijumaa.

2. Jipatie Cd za Ustadh Na'maan kuhusu jinsi Älivyokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifunga mwezi wa Ramadhaan. Na pia Cd za Mawaidha mbalimbali za ma-Duáat wetu.

3. Jipatie nakala ya vitabu vifuatavyo:

- Tafsiri ya Soorah Qaaf. [Sh. Nassor Khamis]
- Namna Ya Swala Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). [Sh. Al-Albaani]
- Damu Asilia Za Wanawake. [Sh. Ibn Uthaymeen]
- Na Risala nyenginezo zenye faida katika Dini.

Utayapata Yote hayo katika Maktaba ya QSS—Mombasa.

wa ishirini na tatu, na wa ishirini na tano, na wa ishirini na saba, na wa ishirini na tisa. Iwapo atakuwa amedhoofika sana au atashindwa kuutafuta katika siku zote za usiku wa witr, basi na ajitahidi kuutafuta katika usiku wa witr za siku saba za mwisho: usiku wa ishirini na tano, na wa ishirini na saba na wa ishirini na tisa. Na Allaah Ndiye Mjuzi aliye bora.

- **Muislamu aitafute vipi Laylatul-Qadr?**

Mwenye kuukosa usiku huu uliobarikiwa wa Laylatul-Qadr basi amekosa kheri nyingi kwani hapana aukosae usiku huo isipokuwa yule aliyekoseshwa kheri zote. Kwahivyo, imependekezwa juu ya Muislamu mwenye hamu yakuwa mtwi'ifu kwa Mola wake na asimame kwa ajili ya kuswali katika usiku huu akiwa na imani na tamaa katika ujira wake, kwani akifanya hivyo, Allaah atamsamehe madhambi yake yaliyotangulia.

Akasema (صلى الله عليه وسلم): "*Mwenye kusimama katika usiku wa Laylatul-Qadr, kwa imani na kutarajia malipo, atasamehewa yaliyotangulia katika masdhambi yake.*"

Imependekezwa kuomba du'aa' kwa wingi katika usiku huo, imepokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba alisema: "Yaa Rasoolallaah! Waonaje lau kama ningelijua ni usiku upi huo wa Laylatul-Qadr, nisemeje utakaponifikia?" Akamjibu: Sema: "*Allaahumma Innaka 'afuwwun, tuhibbul 'Afwa Fa'fu'anne.*" Ewe ndugu yangu! Allaah akubariki na akuafikie katika kumtwi'i Yeye, umekwisha kujua umuhimu wa usiku huu, kwahivyo simama kwa ajili ya ibada katika siku kumi za mwisho, na ujiepusha na wanawake, ukiwaamrisha ahli yako na mambo hayo, na kuzidisha kwenye wakati huo vitendo vya utwiifu na ibada.

Kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) aliyesema: "Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akijikaza saruni (izaar), akishughulika na ibada usiku, na akiwaamsha ahli zake wakati wa usiku wa siku kumi za mwisho." Kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) "Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akijitahidi katika siku kumi za mwisho zaidi kuliko anavyojitahidi katika siku nyengine."

- **Alama za Laylatul-Qadr**

Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliusifu wakati wa asubuhi baada ya Laylatul-Qadr, ili Muislamu apate kujua ni siku gani yenyewe. Kutoka kwa 'Ubayy (رضي الله عنه) aliyesema: "yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Katika asubuhi ifuatayo Laylatul-Qadr, jua huchomoza bila ya miyale, kama bakuli la shaba, mpaka lipande juu. Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema: "Tulikuwa katika mazungumzo kuihusu Laylatul-Qadr katika hadhara aliyokuwepo Mtume (صلى الله عليه وسلم), mara akasema (صلى الله عليه وسلم): 'Ni nani miongoni mwenu aukumbukae (usiku) mwezi unapopanda kisha ukawa kama nusu sahani?"

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) aliyesema: "Amesema Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم): "Laylatul-Qadr ni (usiku) mtulivu, wenye kung'ara, usokuwa na joto wala baridi. Jua hupambazuka asubuhi yake likiwa dhaifu tena jekundu.

I'tikaaf

- **Hikma Yake**

Amesema Ibn al-Qayyim : "Ilipokuwa kutengenea kwa moyo na msimamo wake juu ya njia ya kuelekea kwa Allaah (سبحانه وتعالى) hutegemea jinsi unavyo uelekeza kwa Allaah Peke yake na kuusababisha ugeuke na kumkabili Allaah (سبحانه وتعالى) kikamiliofu. Kwa vile kuharibika kwa moyo hakuwezi kurekebishika isipokuwa kwa kurudi katika njia ya Allaah (سبحانه وتعالى) na uharibifu wake utazidishwa kwa kula na kunywa kupita kiyasi, kuchanganyikana na watu bila ya mipaka, kuzungumza ovyo na kulala sana. Mambo haya huusababisha kuzurura kwenye kila bonde, na kuukatiza kutoka kwenye njia yake ya kuelekea kwa Allaah, kuudhoofisha, kuupotoa au kuukomesha. Miongoni mwa Rehma za Allaah ni kwamba amewafaradhishia wao kufunga, ambako kutakakowakatiza kula na kunywa kwingi, na kuondoa matamaniwa katika moyo ambao ni wenye kupotosha kwenye msafara wake wa kuelekea kwa Allaah (سبحانه وتعالى) Aliifaridhisha kwa uwiano ufaao kama itakavyostahiki katika kumfaidisha mja, kuhusiana na ulimwengu wake na akhera yake, na si kitu cha kumdhuru wala kumuharibia kitu kilicho na maslaha nae. Vilevile akawawekea i'tikaaf, ambayo makusudio yake na msingi wake ni kujifungamanisha nafsi yake na moyo wake kikamilifu kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na kujikusanya mbele Yake. Na kuuweka (moyo huo) faragha na Allaah, na kujikatiza na kushughulika na viumbe. Bali umeshughulika na Allaah peke Yake, aliye epukana na kila aina ya upungufu, kiasi cha kwamba kumkumbuka Yeye, kumpenda Yeye, na kumuomba Yeye huchukuwa mahali pa khofu zote za moyo na ushawishi wake mpaka akaweza kuzihimili hali zote hizo. Kwahiyo, kila jambo alifanyalo linakuwa ni kwa ajili ya Allaah. Mawazo yake yote yakawa ni yenye kumkumbuka Yeye, akawa anawaza jinsi atakavyopata radhi Yake na litakalo sababisha kupatikana mkuruba Wake. Hilo humpelekea akapata umakinifu na Mola wake badala ya watu, kwahiyo, hayo humtayarisha awe kwenye amani na Yeye peke yake katika siku ya upweke kaburini, wakati ambao hakuna mwengine awezae kumpumbaza, wala yoyote awezae kumfariji isipokuwa Yeye. Kwahivyo, hili ndilo lengo kuu la i'tikaaf.

- **Maana Yake**

Maana yake ni kulisimamia jambo; ikasemwa: Yule ambae atakaejilazimisha kukaa msikitini akajilazimisha kufanya ibada ndani ya msikiti.

- **Uwajibu Wake**

Imependekezwa katika mwezi wa Ramadhan na siku nyengine za mwaka mzima, kwani imethubutu yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya i'tikaaf kwa siku kumi (katika mwezi wa) Shawaal. Pia, 'Umar alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Yaa Rasoolullaah, mimi nilikuwa nimeweka nadhiri katika wakati wa Ujahiliyya yakwamba nitafanya i'tikaaf kwa usiku mmoja kwenye msikiti Mtukufu wa Makkah (al-Masjidul-Haraam).*" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia, "basi tekeleza nadhiri yako [na ufanye i'tikaaf kwa usiku mmoja]." Hatahivyo, bora ya i'tikaaf ni katika mwezi wa Ramadhan kutokana na hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه): "*Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya i'tikaaf kwa siku kumi kila mwezi wa Ramadhaan, kisha ulipofika mwaka ambao* Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokufa, alifanya i'tikaaf kwa siku ishirini." Wakati bora ni mwishoni mwa Ramadhaan, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Alikuwa akifanya i'tikaaf katika siku kumi za mwisho za Ramadhaan mpaka Allaah* (سبحانه وتعالى) *alipomchukuwa.*"

- **Shuruti zake**

Haikuwajibishwa isipokuwa msikitini, kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wala msiwaingilie (wake zenu) na ilhali ni wenye kukaa i'tikaaf katika msikiti,"** [al-Baqarah 2:187].
Misikiti iliyotajwa hapa si yoyote kwani imekuja Sunnah iliyo swaheeh ya kuifunga sharti hii. Nayo ni maneno yake (صلى الله عليه وسلم) aliposema: "*Hakuna I'tikaaf isipokuwa kwenye misikiti mitatu.*" Sunnah kwa mwenye kufanya i'tikaaf ni kwamba na afunge kama ilivyopokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله

(عنها

- **Mambo yanayofaa kwa mwenye kufanya I'tikaaf**

Yajuzu kwa aliyekaa i'tikaaf kutoka msikitini kwa ajili ya haja, na anawez kujiegemeza nje ya msikiti kwa ajili ya kuoshwa kichwa chake au kuchanwa nywele zake. Amesema 'Aaisha (رضي الله عنها) "Mtume (صلى الله عليه وسلم alikuwa akiniegemeza kichwa chake alipokuwa (akifanya i'tikaaf) msikitini (na mimi nilikuwa ndani ya chumba changu) na nilikuwa nikimchana (na katika riwaya: nikiziosha) [na kizingiti cha mlango kilikuwa baina yangu mimi na yeye] [na nilikuwa na heidh] na alikuwa haingii nyumbani isipokuwa kwa mahitaji [ya mtu], alipokuwa akifanya i'tikaaf." Inaruhusiwa kwa mwenye kufanya i'tikaaf na kwa wengine kutawadha msikitini kutokana na maneno ya mtu aliyekuwa akimtumikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametekeleza wudhoo' hafifu msikitini." Anaweza kutengeneza hema dogo nyuma ya msikiti kisha afanye i'tikaaf ndani yake, kwani 'Aaisha (رضي الله عنها): alikuwa akimsimamishia Mtume (صلى الله عليه وسلم) hema dogo alipokuwa akifanya i'tikaaf, na hii ilikuwa ni kama alivyoagiza kufanywa. Anaweza kuweka matandiko yake au godoro ndani kutokana na aliyoyapokea Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Yakwamba alipofanya I'tikaaf, huwekewa matandiko au godoro nyuma ya 'Nguzo ya Toba'*."

- **I'tikaaf Ya Mwanamke, Na Kumfanyia Ziyara Mumewe Msikitini**

Yafaa kwa mwanamke kumzuru mumewe anyefanya i'tikaaf, na anaweza kumuaga na kumshindikiza mpaka kwenye mlango wa msikiti. Swafiyyah (رضي الله عنها) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya i'tikaaf [katika usiku wa siku kumi za mwisho wa Ramadhaan], basi nikaja kumtembelea wakati wa usiku [na alikuwa pamoja na wake zake kisha wakaondoka]. Nikazungumza nae kwa muda, kisha nikainuka kwa ajili ya kuondoka, [kisha akasema: *"Usiwe na haraka, kwani nitakushindikiza*." Akainuka na mimi ili anishindikize – na makaazi yake yalikuwa kwenye nyumba ya Usaamah ibn Zayd [mpaka alipofika kwenye mlango wa msikiti uliokuwa karibu na mlango wa Umm Salamah], mara wakapita watu wawili wa ki-Aswaar, walipomuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakakaza mwendo, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *"Polepoleni, kwani huyu ni Swafiyyah bint Huyayy*." Wakasema: "Subhaanallaah (Kutakasika ni kwa Allaah)! Yaa Rasoolallaah!" Akasema, *"Kwa hakika Shaitaan huzunguka ndani ya mwili wa mwana-adamu kama inavyozunguka damu, na mimi nahofia yakwamba ataingiza dhana mbaya*" – au alisema: *"kitu – ndani ya nyoyo zenu*." Inaruhusiwa kwa mwanamke kufanya i'tikaaf pamoja na mumewe au peke yake, kama alivyosema 'Aaisha (رضي الله عنها): "*Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *alikuwa akifanya i'tikaaf katika usiku wa siku kumi za mwisho wa Ramadhaan mpaka Allaah akamukhitari, kisha wake zake wakafanya i'tikaaf baada yake*," Sheikh wetu [al-Albaani] (رحمه الله) amesema: "Na ndani yake kuna dalili ya kuwaruhusu wanawake kufanya i'tikaaf, na hapana shaka yakwamba ni sharuti ipatikane ruhusa ya wasimamizi wao, na kwamba kupatikane usalama wa kutokana na fitna, na kwa kuwa na faragha na wanaume – kutokana na dalili nyingi (zenye kukataza) hayo, na msingi wa fiqh hapa ni kwamba kuepusha ufisadi hupewa kipaumbele juu ya kufanya wema."

[Endelea kutoka Vol. 1, Issue 3

..Saumu ya mwezi wa Ramadhaan]

Hii imethibitishwa kulingana na jinsi amri ilivyoafikiana katika hadeeth ya 'Aa'ishah, kisha amri hiyo ikatiliwa mkazo zaidi kwa kuzidi kuthibitisha kwa njia ya kujumuisha matangazo, na kisha kuzidi kuafikiwa kwa amri yakwamba yule ambae ashakula na ajizuiye kama ilivyokuja katika hadeeth ya Salamah Ibn al-Akwaa' na ile ya Muhammad Ibn Swaifee al-Answaaree aliyesema: "*Alitujilia Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *katika siku ya 'Aashooraa' akasema: Jee, mumefunga katika siku yenu hii? Basi baadhi yao wakasema, "Ndio" na baadhi nyengine wakasema, "Laa". Akasema: basi ikamilisheni siku yenu hii. Na akawaamrisha wawatangazie watu waliokuwa katika vijiji vya Madeenah yakwamba waikamilishe sehemu iliyobaki ya siku*."

Tafauti za kauli zinaondoshwa na kauli ya Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) pindi ilipofaradhishwa Ramadhaan, saumu ya 'Aashooraa' iliachwa. Na vilevile kauli ya 'Aa'isha (رضي الله عنها) Pindi ilipokuja saumu ya Ramadhaan, ikawa Ramadhaan ndiyo Faradhi, na 'Aashooraa' ikawachwa. Mapendekezo ya kufunga saumu ya 'Aashooraa' yamebaki palepale – kwa hakika kuna *Ijmaa'* (maafikiano kwa ujumla) yakwamba imependekezwa kama alivyosimulia al-Haafidh katika al-fat-h (4/246) kutoka kwa Ibn 'Abdul Barr.

Kwahivyo, yamkinika hukmu hiyo imebaki palepale, kuonyesha yakwamba kilichofutwa ni kufaradhishwa kwake – na Allaah ndiye Mjuzi Mkubwa. Wengine wanasema: Iwapo ilikuwa ni faradhi basi baadae ilifutwa, na hukmu zilizofungamana nayo pia zilifutwa. Lakini ukweli ni kwamba ahaadeeth kuhusu 'Aashooraa' zinaashiriya nukta nyingi:

a) Saumu ya 'Aashooraa' ni faradhi.

b) Yakwamba mtu ambae hana niya ya kufunga saumu ya faradhi kabla ya mapambazuko ya al-fajiri kwa ajili ya kughafilika – jambo hilo halitoharibu saumu yake.

c) Mwenye kula na kunywa, kisha akatanabahi, na aendelee kujizuiya katika hali hiyo kwenye wakati uliobaki wa siku na wala hatowajibika kuilipa siku hiyo.

Kilichofutwa katika hayo ni nukta ya kwanza, (a), na ikawa ni jambo lililokokotezwa kama ilivyotangulia – na kutokana na uhakika yakwamba jambo hilo lilifutwa haimaanishi yakwamba hukmu nyengine pia zilifutwa – Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

Pia wanatumia kama dalili, hadeeth iliyopokewa na Abu Daawud (no. 2447) na Ahmad (5/409), kutoka kwa Qataadah: kutoka kwa 'Abdur-Rahmaan Ibn Salamah: kutoka kwa mjombake: yakwamba Aslam alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Jee, mumefunga katika siku yenu hii? Wakasema: 'Laa', Akasema: Basi jizuiyeni katika siku yenu hii kisha muilipe*."

Hatahivyo, hadeeth hii ni *Dha'eef* iliyo na ila aina mbili:

i) Hakika yakwamba huyu 'Abdur-Rahmaan Ibn Salamah ni mtu asojulikana (*Majhool*). Akasema adh-Dhahabi kumuhusu mtu huyu katika *al-Meezaan* (2/567): "Hajulikani." Al-Haafidh akasema katika *at-Tahdheeb* (6/239): "Hatumjui hali yake," Ibn Abee-Haatim akamtaja katika *al-Jarh wat-Ta'deel* (5/288) bila ya kusema chochote dhidi yake au kumuhusu yeye."

ii) na ndani yake '*an'anah* ya Qataadah ambaye ni *mudallis*.

Wakati Wa Kuanza Na Kumaliza Saumu

Walipokuwa wakifunga Maswahaba wa Mtume asiyekuwa akijua kusoma wala kuandika na wakati wa kufungua saumu unapoingia, wao hula, na hunywa na huingiliana na wake zao maadamu hawakupata lepe la usingizi. Ikiwa mmoja wao amelala kabla ya kula chakula cha jioni basi ilikuwa haifai kufanya lolote katika hayo mpaka jioni ya siku ifuatayo. Kisha wakagubikwa na Rehma ya Mola wao, Mwenye nguvu, Aliye mtoaji, wakapewa ruhusa na likawafurahisha jambo hilo, kimeelezwa kisa hicho katika hadeeth ifuatayo:

[Endelea kwenye Makala Yajayo]

... Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-'Uthaymeen (رحمه

[Endelea kutoka Vol. 1, Issue 3]

Mfano wa Kwanza: Imemjia mwanamke ada yake mapema baada ya kutwa kwa jua. Hatahivyo, alikuwa yuko twahara kwa muda wa wakati unaomtosha yeye kupata rakaa'ah moja kutoka kwenye swala ya Maghrib. Siku atakapo twahirika tu, atalazimika kuilipa swala yake ya Maghrib.

Mfano wa Pili: Ada ya mwanamke ilisimama kabla ya kucha kwa jua akiwa ndani ya wakati unamtosheleza yeye kuipata rakaa'ah moja ya swala ya Al-Fajr (Asubuhi). Mara tu atakapojitakasa au kujitwahirisha, basi itampasa yeye ailipe hiyo swala ya Al-Fajr.

Katika mifano yote hiyo miwili, iwapo wakati haumtoshelezi yeye kupata rakaa'ah moja, basi hatolazimika kuswali kwa sababu, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلّم):

"Atakaepata rakaa'ah moja katika swala (katika wakati wake wa kisheriya), basi huyo ameipata swala. "

Mas'ala: Tuseme mwanamke aweza kupata rakaa'ah moja ya swala ya 'Asr katika wakati wake wa kisheriya. Jee, atawajibika yeye kuswali swala ya Adhuhuri (Dhuhr) pamoja na swala ya 'Asr? Au iwapo mwanamke aweza kupata rakaa'ah moja ya swala ya 'Ishaa' katika wakati wake wa kisheriya, Jee atawajibika yeye kuswali swala ya Maghrib pamoja na 'Ishaa'?

Kuna ikhtilafu miongoni mwa wanavyuoni kuhusu mas'ala haya. Hatahivyo, msimamo wa sawa ni kwamba atatekeleza lile aliloweza kupata katika swala makhsusi, yaani: Swala ya 'Asr na 'Ishaa' peke yake. Hii imetokamana na hadeeth ya bwana Mtume (صلى الله عليه وسلّم): "Yoyote ambae atakaepata rakaa'ah moja katika swala ya 'Asr kabla ya kuzama kwa jua, basi huyo ameipata 'Asr." (Imeafikiwa) . Mtume (صلى الله عليه وسلّم) hakusema "basi yeye mke/mume ameipata swala ya Dhuhr na 'Asr!". Hakutaja yakuwa ni lazima kuswali Swalaat adh-Dhuhr. Huu ndio msimamo wa madh-hab za Imaam Maalik na Imaam Abu Haneefah.

Mas'ala: Wakati wakiwa katika ada zao za mwezi, haikukatazwa kuleta Dhikr (Takbeer, Tasbeeh, Tahmeed), kutamka Bismillaah kabla ya kufanya jambo lolote (kula, kunywa, n.k) kusoma hadeeth, kuzungumzo kuhusiana na Uislamu, Kumuomba Allaah (Du'ah), na kusikiliza Qur'an isomwapo. Imethubutu kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلّم): "*Alikuwa akilala juu ya paja langu na huku akisoma Qur'an, haliyakuwa mimi nilikuwa katika ada yangu (heidh)*."

Vilevile Umm-'Atiyyah alipokea yakwamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلّم) akisema: "*Watoke wanawali, na watawa, au wanawali watawa, na wenye heidh washuhudie kheri na dua za Waumini, lakini wenye heidh hawaswali, bali wajitenga kando*."

Mas'ala: Usomaji wa Qur'an kwa mwanamke, emma kwa kuitazama au kwa moyo, bila ya kupepesa ulimi wake inaruhusiwa. Wanavyuoni wengi wanaonelea yakwamba hilo halikukatazwa kwake kuisoma kwa kuitamka. *Imaam al-Bukhaari, Ibn Jareer at-Tabaree na Ibn al-Mundheer, Imaam Maalik na Imaam ash-Shaafi'ee* (mojawapo ya maneno yake ya awali) rai yao ni kwamba inaruhusiwa kwake kuisoma Ayah (kifungu cha maneno ya Qur'an). Shaykh Ul Islaam *Ibn Taymiyyah*, amesema: "Kimsingi, hakuna Sunnah yenye kumzuiya asisome Qur'an. 'Hadeeth' yakwamba: "*Haifai kwa mwanamke mwenye heidh au mwenye Janaba kusoma chochote katika Qur'an.*"

Hii ni hadeeth dha'eef kama ilivyoafikiwa na wanavyuoni wa 'ilmu wa hadeeth. Kwa hakika wanawake katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلّم) walikuwa wakipata ada zao za kila mwezi. Lau kama wangelikuwa wameharamishiwa usomaji wa Qur'an (kama ilivyo katika swala), basi Mtume (صلى الله عليه وسلّم) angeliwadhihirishia Ummah wake na wake zake wangeliyajua hayo na wangeliyasambaza mafunzo hayo kwa watu. Kwa vile hakukuwa na yoyote aliyesimulia makatazo yatokayo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلّم) kuhusu mas'ala haya, basi haiwezekani kuharamishwa haswa ikiwa yajulikana yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلّم) hakuharamisha jambo hilo katika wakati ambao heidh ilikuwepo. Kulingana na hali ilivyo, usomaji kwa kutamka kwa ulimi si Haram (makatazo ya kisheriya). Muandishi amesema, "baada ya kujua ikhtilafu miongoni mwa wanavyuoni kuhusu mas'ala haya, basi ni jambo la sawa kwa wanawake wenye heidh wasiisome Qur'an kwa ndimi zao isipokuwa ikiwa ni dharura k.m, (kwa mfano), akiwa ni mwalimu au ikiwa anajitayarisha kwa mitihani."

Ya Pili: Heidh na Saumu .

Ni haram kwa mwanamke mwenye heidh kutekeleza aina zote za saumu: saumu za faradhi au za Sunnah. Hatahivyo, ni waajib kuzilipa saumu za faradhi kama ilivyofafanuliwa na 'Aaisha (رضي الله عنهما): "Tuliyapitia hayo (huo muda wa ada), na tukaamrishwa kulipa (yaani; kufidia) hizo saumu, lakini hatukuamrishwa kuzilipa swala" (Imeafikiwa).

Iwapo itamtokea mwanamke ada yake ya mwezi haliyakuwa amefunga, basi funga yake haitofaa hata kama damu yake imeanza kutoka muda mchache kabla ya kutwa kwa jua. Ikiwa siku hiyo ni mojawapo ya masiku ya kuwajibika kufunga, basi itamlazimu nkuilipa siku hiyo pindi atakapotwahirika. Ikiwa katika siku yake ya kufunga alikuwa akijisikiya kama kwamba amekurubia kupata ada yake, lakini ukweli ni kwamba haikumjia damu yake mpaka baada ya kutwa kwa jua, basi funga yake itakuwa imekamilika na haikukataliwa kulingana na rai iliyo sawa kuhusiana na mas'ala hayo. Hii ni kwa sababu hakuna hukmu kuhusu damu ikiwa ndani ya mwili wa mwanamke, na pia alipoulizwa Mtume (صلى الله عليه وسلّم): "Jee, itamlazimu mwanamke kuoga baada ya kuota ndoto (ya kimapenzi)?" akajibu: "Naam, ikiwa ataona chepechepe."

Kwahiyo, Mtume (صلى الله عليه وسلّم) akashurutisha hukmu juu ya kuonekana kwa chepechepe na wala hakuishurutisha juu ya kumwagika kwake (kutoka ndani hadi nje). Vilevile kuhusu mas'ala ya heidh, utendakazi wa hukmu yake ni pindi itakapo-onekana (kudhihiri) chepechepe.

Mas'ala: Ikiwa ada ya mwanamke itaendelea mpaka baada ya kupambazuka (Fajr), basi hakuna saumu itakayokubaliwa kutoka kwake katika siku hiyo hata kama atatwahirika muda mchache baada ya kupambazuka.

Mas'ala: Ikiwa atatwahirika kabla ya Fajr na akafunga, basi kufunga kwake ni sawa hata kama alichelewa kuoga josho la twahara mpaka ulipoingia wakati wa Fajr. Hii ni sawa na hali ya mtu aliyekuwa kwenye Janaba. Iwapo yeye (mume/mke) alinuiliya kufunga na akawa hakuoga mpaka baada ya Fajr, basi saumu yake (mume/mke) itakuwa ni sawa. Hii ni kulingana na hadeeth ya 'Aaisha (رضي الله عنهما) aliyesema: "*Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلّم) akiamka akiwa katika hali ya Janaba* (baada ya kujamiiana na wake zake) *na akifunga katika mwezi wa Ramadhaan*."

[Endelea kwenye Makala Yajayo]

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفرقيا

Tuko katika Tovuti

http://www.qssea.net